## SIFA ZA AKILI ZINAZOHITAJIKA

## (AKILI TIMAMU ZENYE AFYA BORA)

Katika hoja hii, mara nyingi inakuwa ni vigumu sana kuainisha ipi ndio akili sahihi, ambayo inakubalika kuwa ndio akili timamu au akili bora. Au akili yenye sifa zipi ndio tuikubali kuwa hii ndio akili inayohitajika, au tusema **mtu huyu ana akili nzuri.?**

Kwa kawaida kila mtu huwa ana akili zake, na zinamsaidia kwa kiwango chake. Lakini kwakuwa tupo katika somo maalumu la kuongeza akili au la kumfanya mtu awe na akili nyingi zaidi, hatuna budi kuelezea kwa kina viwango au sifa za akili ambazo mtu akiwanazo inafaa kusema kuwa ana akili inayohitajika.

**Sifa za akili zinazohitajika(Akili timamu zenye afya bora)**

**1. Ina uwezo wa kufumbua matatizo yake.** Akili inayohitajika, lazima iwe na uwezo wa kutatua au kufumbua matatizo yake. Kazi ya akili ni kutoa ufumbuzi wa matatizo, au kutoa msaada wa jinsi ya kufanya au kufanikisha jambo fulani. Akili timamu, linapotokea tatizo, hutoa njia ya kulitatua. Katika maandiko ya Biblia inabainisha aina za akili kama tunavyonukuu katika kitabu cha **Zaburi 111:10** *Kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima, Wote wafanyao hayo wana akili njema, Sifa zake zakaa milele.*

Tunapoona maanadiko yanataja kama kuna akili njema, basi pia tunaamini kuna akili nyingine ambazo ni mbaya. Lengo tujue kuwa, sio kila akili

inafaa, au sio kila akili ni nzuri. Yafaa tujue kuwa kuna aina nyingi za akili, lakini tunachokitafuta kujua akili zilizo bora zaidi ya nyingine.

Hakuna maana ya kuwa na akili ambayo ukiwa na tatizo inashindwa kutoa ufumbuzi. Kama una **kalikuleta**(kikokotoo) lakini unapoipa hesabu haitoi majibu au inachanganyikiwa je kuna maana gani ya kuwa na **kalikuleta** kama hiyo? Ninacho maanisha hapa ni kukujulisha kuwa, ubora wa akili ni kazi zake inazofanya au iwapo zitamsaidia aliye nazo kufumbulia matatizo yake magumu. akili ni **"problems solver:**

Kwa hiyo basi, inafaa tuupime ubora wa akili katika uwezo wake wa kutoa ufumbuzi kwa mwenye nazo. Neno akili tunaweza kuliita jina lingine nalo ni **"Utambuzi"** Utambuzi, ni hali ya kugundua au kujua baada ya kutokujua, au kufichua kile kilicho fichika. Akili lazima iweze kutambua vitu ambavyo kwa kawaida ni vigumu kuvijua au kuvipatia utatuzi.

**Sababu za watu wengi kujinyonga au kukata tamaa.** Tendo la kujinyonga, ni moja ya matatizo ya akili au udhaifu wa akili, au ni moja ya tatizo la kukosa ubora wa akili. Unapoona mtu ameamua kujinyonga, inamaana amekosa majibu ya tatizo lililomtokea. Pale mtu akili zake zikishindwa kutoa ufumbuzi wa matatizo ambayo mtu yamemtokea, kinachofuata ni kukata tamaa na baada ya kukata tamaa ni kujiua au kufanya maamuzi mengineyo ambayo si maamuzi sahihi.

Ukiangalia Mikoa mingi **inayoongoza watu kujinyonga** au kuwa na mauji mengi kwa watu wasiokuwa na hatia aidha kwa imani za kishirikina, utabaini pia kwa kawaida wakaazi wake **wana uwezo mdogo wa**

**kufikiri(wajinga)** Au wengine wanawaita **washamba**. Au kuna hali fulani ya **wehu**.

**Kukata tamaa.**

Kukata tamaa **"giveup"**ni tendo la kupoteza muelekeo, kukosa majibu, kutokuwa na tumaini tena **"hopeless"** Mara nyingi mtu anayekata tamaa ni yule aliyepoteza shabaha ya malengo yake, au pale makusudi yake yanapogonga mwamba.

**2. Sifa ya pili ya akili, hutoa majibu (Matokeo) sahihi iwapo yatapimwa na wengine.** Akili iliyo njema ni ile ambayo matokeo au kile ilichofanya au kuamua kikiangaliwa au kupimwa na wengine hubainika kuwa kipo sahihi au kimefanyika katika maamuzi yaliyo sahihi. Akili haipaswi kuwa na majibu yasiokubalika na wengine, mtu yoyote asiyejali viwango vinavyofaa kwa watu wote, huyo hawezi kuwa na akili sahihi.

Iwapo utaona mara kwa mara maamuzi yako hukataliwa na watu, au hubezwa, yafaa utambue aidha una akili nyingi nno kuwapita wao wanaokubeza au wewe ndio mwenye tatizo katika maamuzi yako. Iwapo utakuwa na maono makubwa ambayo yanawapita uwezo wao wa kufikiri watu ulionao, inawezekana wakashindwa kuyakubali, lakini haina maana haupo sahihi.

Lakini mara zote mtu mwenye akili njema ana ujuzi mzuri wa kuyatafsiri maono au maamuzi yake, ili yaweze kueleweka hata kwa wale ambao ni wajinga. Tunarejea kwenye hoja yetu ya msingi, kuwa mwenye akili njema ni lazima maamuzi yake yakubalike au yaeleweke na wengine. Akili ni

uwezo wa kupima, au **ni kitu kinachotoa jawabu lililokadiriwa vizuri,** aidha akili ni kiwango sawazishi, kinachotoa uuwiano nzuri. Akili ni nuru inayomulika kile kilichokuwa hakionekani kionekane katika uhalisia wake. Mara zote akili inatoa majibu yatakayowafanya watu wakubali kuwa kilichofanyika ndio haswa.

**3. Sifa ya tatu ya akili ni, uwezo wa kuelewa yaliyo sahihi.** Kwa kawaida binadamu ana njia kuu mbili ya majawabu au jinsi ya kufanyia kazi jambo au mambo. Kuna **(input)** na (**output),** nikiwa na maana mtu ana njia ya kutoa yaliyofanyiwa kazi ndani kwenda nje, na yaliyofanyiwa kazi nje (na watu wengine) kwenda ndani yake.

Nikiwa na maana mtu unapotoa maamuzi yako ambayo umeyafikiri na kuwashirikisha au kuyawasilisha kwa watu wanaopokea hiyo inahesabika ni kutoa, lakini iwapo utapokea kutoka kwa mtu au watu wengine ***(Kusikiliza shauri au maamuzi)***hiyo inahesabika ni kuingiza.

Katika mada hii ya **uwezo wa kuelewa yaliyo sahihi,** lengo ni kuendelea kujua au nafasi ya pili ya akili katika kufanyia kazi yale ambayo watu wengine wameyafanya au kuamua au kushirikisha, ni jinsi gani unaweza kupima na kujua kilicho wasilishwa kwako ni sahihi au hakipo sahihi, ni jinsi gani unaweza kuelewa pale unapoeleweshwa jambo fulani?

Mtu mwenye akili sahihi, kwa kawaida ana **uwezo wa kuelewa pale anapoeleweshwa** au anaposhirikishwa mawazo na watu wengine, *anaweza kujua kwa usahihi alichoshirikishwa kama ni sahihi au sio sahihi.* Iwapo unamuona mtu anapenda au anashinikiza mara kwa mara mawazo yake tu

ndio yakubalike au watu wayafuate**(Au pia anakubali kila kitu atakachoshirkishwa),** bila kujali usahihi wake, inafaa kujua kuwa mtu huyo ana tatizo la akili**(Akili yake haipo sawa),** tunaweza kutambua akili ya mtu kuwa ni mbaya au inashida iwapo huyo mtu atakuwa anatoa maamuzi au atafanya mambo yasiyo katika hali iliyo sawa**(wrong decision is one of indicate of mental problems).**

Kama uliwahi kuongea na mtu kwa muda mrefu bila ya kufikia muafaka, umetumia uwezo wako wote ambao unaamini kwa kawaida mtu yoyote angeweza kueleawa, lakini yeye haelewi au haafiki. Na iwapo utamuelezea mtu mwingine shauri hilo, huyo mtu mwingine atakubaliana na wewe.

Au ikiwa yule aliyeshindwa kukuelewa akiitwa kwenye kikao cha watu wengi ili wawasikilize, na baada ya kuwasikiliza itabainika kuwa wewe upo sahihi na yeye(aliyekuwa hakuelewi) ndiye hayupo sahihi. Tambua kuwa huyo mtu ana tatizo la kuelewa, yaani akili zake zina shida.

Wakati fulani usipojua mambo ya matatizo ya akili unaweza kupoteza muda wako kwa kuongea na watu au kuwaelewesha na wasikuelewe ukadhani wanafanya makusudi, kumbe, ni shida ya akili zao hazipo timamu.

**Akili timamu,** kwa kawaida pia, zinauwezo mzuri wa kuelewa yale yanayoshirikishwa. Jipime akili zako kwa kuangalia ni jinsi gani unawaelewa watu wengine hasa wanapokushirikisha au kukushauri mambo ambayo kwa kawaida sio mabaya au yaliyo sahihi. Iwapo utakuwa

na tabia ya kupinga au kukataa hata yaliyo sahihi, basi tambua una tatizo la akili.

**4. Sifa ya nne ya akili ni, kuwa mbunifu (Craetivity).** Akili yoyote njema***(Akili yenye uwezo mkubwa)*** kwa kawaida inakuwa na sifa ya ubunifu. *Ubunifu ni hali ya kujiongeza baada kuona njia ya kawaida pengine inaweza kukosa matokea mazuri,* ubunifu unatoa jawabu mbadala. Kwa kawaida mtu mwenye akili ndogo au mwenye uwezo mdogo kiakili huwa anakosa ubunifu.

Ubunifu ni moja ya tunda la mtu kuwa na uwezo mkubwa kiakili. ***Bila shaka ndio kitu adimu kinachokosekana kwa watu wengi.*** Mbunifu si mtu wa kulalamika bali ni mtu wa kutoa majawabu ya kushangaza pale wengine wakishangaa nini cha kufanya.

**5. Sifa ya tano ya akili, ni kuwa na kiwango kidogo cha hasira "Kuwa na hasira kwa mbali"**

Sifa ya akili njema kwa kawaida huwa na ***hasira kidogo au hasira kwa kiwango cha chini,*** au kuwa na hasira za mbali*(kutokuwa na tabia ya kukasirika harakaharaka)* Tukiangalia katika maandiko Matakatifu ya Biblia katika kitabu cha Mithali Inasema hivi , 14:29 *Asiye mwepesi wa hasira* ***ana fahamu nyingi****; Bali mwenye roho ya hamaki hutukuza upumbavu.*

Mtu asiye mwepesi wa hasira inamaana ana uwezo wa kujizuia au kuzuia hasira zake. Kitu kinachoweza kumsaidia mtu kuzuia hasira zake ni akili au fahamu nyingi. Mtu anapokuwa na hamaki, au hasira za haraka, hiyo

inaashiria tatizo la akili**(uwezo mdogo wa akili)** Hasira ni matokeo ya ukosefu wa upambambanuzi mzuri wa mambo.

Hakuna mwanadamu aliyekosa hasira kabisa, isipokuwa tunazungumzia hasira iliyozidi, au hasira ya haraka. Kwa mujibu wa kanuni nyingi za watu wanaotafsiri maana ya akili au uwezo wa akili, wanaongelea kuwa na uwezo wa kujizuia hasira, unahitaji akili nyingi**(Kuwa na uwezo wa kufikiri na kuamua vema).**

Mara zote mtu mwenye hasira nyingi, au mtu anayehamaki au kukasirika harakaharaka tunamuweka katika kundi la watu wenye matatizo ya akili***(uwezo mdogo wa akili, au ana tatizo lingine la ungonjwa wa akili au ana dalili zinazoelekea kuwa na matatizo ya akili).*** Yafaa upime uwezo wako wa akili kwa kuangalia ni jinsi gani unazuia hasira zako.

**6. Sifa ya sita, husaidia mwili kufanya kazi vizuri na kuuweka mwili katika muonekano wake wa kuvutia.** Akili kwa kawaida kabla ya kuonyesha mambo makubwa ambayo mtu angeyafanya kupitia akili, kwanza zisaidie mwili wa mtu binafsi kufanya kazi vizuri au akili zitoe msaada wa mwili kujihudumia.

Ninaposema akili zitoe msaada wa mwili kujihudumia nina maana hii, vile mtu anavyoweza kujipenda au kujijali. Kama utaona mtu hajipendi au hajijali, basi hiyo inatosha kuwa sababu ya kumuweka mtu huyo katika kundi la mwenye mapungufu ya akili.

Mtu mwenye akili nzuri, akili zake zitatoa msaada kwa mwili kujihudumia kwa usafi wa meno, mwili, usafi wa nyumba, uwanja, usafi wa nguo,

nywele, kwenda chooni kujisaidia, kulala, na kula chakula. nk. Akili zitoe msaa katika kazi kuu za mwili kama zifuatazo.

**1. Kutambua mahitaji** ya kila siku ya mwili na kisha akili kuoongoza mwili kuyatimiza.

**2. Akili kuusukuma mwili kujihudumia.** Kwa kawaida mwili hauna maamuzi yake binafsi, pale akili zikiamua kufanya kitu fulani hata kama mwili umechoka utasukumwa tu na utafanya.

**3. Huondoa uvivu wa mwili.** Kwa kawaida tumezoea kuona au kusema ***mtu fulani ni mvivu au hapendi kufanya kazi,*** bila kujua nini chanzo cha uvivu. Chanzo cha uvivu ni akili. Akili ikiwa haifanyi kazi vizuri mtu atajikuta hapendi kufanya kazi. Mara zote tunapowaona watu wanasumbuliwa na hali ya uvivu tujue kuwa hiyo inatokana na akili kutokufanyakazi zake vizuri.

Kwa hivyo basi, tunapaswa kujua mtu akiwa na akili inayofanyakazi vizuri hawezi kuwa mvivu. Kwa maana akili ndio inayoulazimisha mwili ufanye kazi. Hali ya kupenda kazi ni moja ya dalili muhimu za kuashiria kuwa na uwezo mzuri wa kiakili.